

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
Tarehe 12 Januari 2008**

Waliohudhuria

Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishehe
Aseli Wilison
Dominata Rwechungura
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Idd Selemani
Kibwana Mohammad Msiga
Musa Athumani Lahi
Rashidi Saidi Karanji
Yusufu Juma

Mkutano na Wizara ya Miundombinu

Elaine aliwapa barua wizara ya Miundombinu idara ya usalama barabarani kuomba tukutane nao na wamekubali kutana na watu watano wa UWABA jumatatu saa nne asubuhi. Alifanya marekebisho ya maada yetu na pia wanachama wengine walipitia na walifanya marekebisho. Wanachama walichagua Mejah, Elaine, Juma, Rashid na Yusufu kuhudhuria mkutano huu.

National Institute for Transportation (NIT)

Elaine alienda ofisi ya Bwana Wemba. Alisema ni nzuri washiriki katika semina wapate chai ya asubuhi kwenye canteen ambayo ni Tsh 800 kila mtu. Tulikubali kutumia hela ya UWABA kwa ajili ya hiyo gharama.

Filbert aliuliza kama washiriki waje na kalamu na karatasi. Elaine alisema atatafuta taarifa kama chuo anatupa an tunakuja nazo, na atatoa taarifa kwa message ya simu.

Mwanachama walipendekeza tuwe na kamera tuwe na kumbukumbu ya semina.

Mpaka sasa wanachama 21 wamejiandikisha kwa semina na tuliambiwa tusizidi watu 50.

Juma alisema ana orodha ya wapanda baisikeli wanaokaa mkoa wa Pwani lakini wanakuja Dar es Salaam mara nyingi kwa baisikeli, ambao wataweza kupenda kushiriki katika semina. Atawauliza na atatoa orodha ya wanaopenda kuhudhuria.

Tulikubali kutana ofisi ya UWABA saa moja kamili jumamosi na tunaweza kwenda semina pamoja.

Wamba Memorial Fund

Elaine alisema amepata email kutoka Wamba Memorial Fund na wamekubali maombi yetu ya hela ya mradi ya usalama barabarani kwa wapanda baisikeli. Wanachama walifurahi sana. Wamba Memorial Fund walisema watatutumia mkataba na taarifa ya vipi tutapata ile hela. Aidha Elaine aliwapa taarifa HUWATA na Ben Bikes.

TANROADS

Tulipata jibu la barua yetu kutoka TANROADS ambayo ilikuwa na tarehe ya Novemba lakini tulipata Januari kwa kufuatilia na kuchukua kutoka ofisi zao – inaonekana hwajatutumia kwa posta. Barua inasema kwamba wapanda baisikeli watakuwa na sehemu maalum kwenye barabara za Sam Nujoma na Kilwa ambayo si sawa na service road. Lakini kwenye hizi barabara sehemu ambazo zimejengwa tayari njia ya baisikeli haionekani. Elaine alitembelea TANROADS na aliongea na mfanyakazi wa idara ya usalama barabarani na alisema atatafuta michoro.

Umoja wa Ulaya

Elaine aliongea na engineer ya barabara ofisi za Umoja wa Ulaya. Baada ya hiyo aliandika barua kuwaomba taarifa kuhusu sera za kutafuta maoni ya wanaotumia barabara, na sera kuhusu sehemu za wapanda baisikeli na watembea kwa miguu kwenye barabara ambazo Umoja wa Ulaya wanalipia. Juma atapeleka barua wiki hii.

Barabara ya Morogoro

Ally Saidi Mohammed alitoa photocopy ya michoro ya barabara ya Morogoro na nakala ipo ofisini. Tulikubali wanachama watasoma na watatoa maoni yao.

Guta

Ally Saidi Mwishehe alileta Tsh 7,000 kwenye mkutano wa wiki jana na Tsh 7,000 zaidi kwenye mkutano wa wiki hii.

Polisi wa trafiki na sheria za barabara

Elaine aliprint nakala ya Road Traffic Act na marekebisho ya Road Traffic Act. Ataweka alama kwenye sehemu zinazohusika wapanda baisikeli.

Juma alipeleka barua polisi wa trafiki lakini walisema tuwaite kwenye mkutano siyo kutana ofisini kwao. Elaine ataenda pale kupata taarifa ya vipi tuendeleo.

Bike Nouveau Fabrique

Elaine alileta kadi ya kushukuru na wanachama walisaini. Mejah atakapo maliza T-shirts atawatumia kadi pamoja na T-shirt.

Sanduka la Posta

Elaine na Juma walichukua hela ya Tsh 23,000 kutoka benki na pamoja na Tsh 7,000 ya guta Juma alilipa ada ya sanduka la posta ya Tsh 30,000 ya mwaka 2008.

Shughuli inayobaki

Kazi ambayo bado haijamalizika: kuandaa karatasi kwa ajili ya ofisi (Elaine), kutengeneza bao za tangazo zinazobaki (Ally Saidi Mohammed), kununua helmeti na kutengeneza T-Shirts (Mejah).

Majibu ambayo bado hatujapata: Serikali ya Jiji, Polisi ya Trafiki